



Mpango wa Makazi ya Kibinadamu

MABADILIKO YA HUDUMA KUTOKANA NA COVID-19

Usaidizi chini ya Mpango wa Makazi ya Kibinadamu unaendelea kupatikana kwa wateja wakati wa kipindi cha janga la COVID-19. Hata hivyo, njia ambayo huduma zinawasilishwa inaweza kubadilika kulingana na ushauri rasmi wa afya.

Tafadhali wasiliana na mtoaji wako wa **HSP service provider** moja kwa moja kujadiliana mipangilio mipya.

Jifunze kuhusu **COVID-19 na dalili zake (symptoms)**.

Mapitio

Mpango wa Makazi ya Kibinadamu (HSP) unatoa msaada kwa washiriki wa kibinadamu ili kujenga ujuzi na maarifa unaohitajika kuweza kujitegemea na kuwa wanachama hai wa jamii ya Australia.

HSP inawasilishwa kwa niaba ya Serikali ya Australia na watoa huduma kote nchini Australia. Kushiriki katika HSP ni hiari na huduma zinawasilishwa kwa wateja kupitia mbinu wa usimamizi wa kesi ya mahitaji.

Watoa huduma wa HSP wanaunga mkono wateja kufikia matokeo katika maeneo yafuatayo ya kipaumbele kama msingi wa makazi yenye mafanikio:

- Ajira
- Elimu na mafunzo
- Huduma za lugha
- Nyumba
- Kusimamia fedha
- Afya ya ustawi wa kimwili na kiakili
- Ushiriki na mitandao ya jamii
- Kazi za kifamilia na usaidizi wa kijamii
- Haki

HSP imeundwa kufanya kazi kwa pamoja na huduma zingine za makazi na za kawaida. Ina lengo kubwa kwa wateja kusaidia kujifunza Kiingereza na kupata ujuzi muhimu wa elimu na wa ajira kwa kutambua kwamba matokeo mazuri katika maeneo haya husaidia wahamiaji wa kibinadamu kuunganishwa katika maisha ya Australia.

Maeneo ya ofisi za watoa huduma wa HSP na maelezo ya mawasiliano yanapatikana hapa **[hapa](#)**.

Ustahili

Wakati mtu mmoja anapewa moja ya viza zifuatavyo kwa makazi nchini Australia, hutumwa na Idara ya Mambo ya Ndani kwa mtoa huduma wa HSP kupata msaada chini ya HSP baada ya kuwasili kwao nchini Australia.

- Viza ya wakimbizi (aina ya daraja 200, 201, 203 and 204); na
- Viza ya Mpango wa Kimataifa Maalum wa Kibinadamu (daraja 202) (ukiondoa washiriki wa Mpango wa Msaada wa Jamii).

Huduma

Mameneja wa kesi za HSP hufanya kazi wakishirikiana na wateja ili kuendeleza mpango wa usimamizi wa kesi na kutoa mfuko wa huduma ambazo hulengwa na mahitaji yao yaliyotambuliwa.

Huduma ni pamoja na msaada wa mapema wa vitendo kama vile:

- mapokezi pale uwanja wa ndege
- malazi wanapowasili na kuelewa nyumba ya kupanga
- utoaji wa chakula cha kwanza na vitu muhimu
- msaada wa kujisajili na Centrelink, Medicare na Benki
- kushughulikia mahitaji ya haraka ya afya
- maelekezo ya nini cha kufanya katika hali ya dharura na jinsi ya kufikia huduma za ukalimani
- mwelekeo wa huduma za eneo hilo.

Huduma zingine zinazopatikana ili kusaidia wateja kufikia matokeo yao ya makazi ni pamoja na:

- uwasilishaji wa mpango wa Mwelekeo hapohapo ambao hujenga maarifa ya wateja kuhusu njia ya maisha na maadili ya Australia
- msaada wa chanzo cha makazi ya muda mrefu
- kusaidia kufikia huduma za tawala, ikiwemo huduma za usaidizi wa afya na familia
- miunganisho kwa vikundi na shughuli za jamii za eneo
- kusaidia kujisajili na Mpango wa Kiingereza wa Wahamiaji Watu Wazima (AMEP) na kuhudhuria masomo
- kusaidia kujiandikisha katika elimu na mafunzo muhimu na kutambua ujuzi pamoja na sifa kabla ya kuwasili
- msaada wa kujihusisha na huduma za ajira, kutekeleza mikakati ya ajira na kupata huduma za msaada kwa ajili ya kuanzisha biashara.

Watoa huduma wa HSP pia wanaweza kuwezesha kuwasilishwa kwa maombi ya programu kwa Huduma ya Bure ya Kutafsiri (FTS) kwa wateja wanaostahili FTS ambao hawawezi kuwasilisha kwenye mtandao.

Kutoka kwenye HSP inategemea na wateja kufikia matokeo ya makazi yaliyobainishwa katika mpango wao wa usimamizi wa kesi. Kwa wateja wengi, matokeo haya yatafikiwa katika miezi 6 hadi 18 ya kuwasili nchini Australia.